


Sokwe alimkuta  
Mamba kando ya ziwa.




Akamwuliza  
Mamba,  
"Unaishi wapi?"

Mamba  
akamjibu, "Ziwani."




Mamba  
akamwuliza,  
"Wewe unaishi wapi?"

Sokwe akamjibu,  
"Kwenye miti."




Mamba akataka  
kumjua Sokwe zaidi.

Akamwuliza,  
"Unaweza  
kuogelea?"



"Siwezi," Sokwe  
akamjibu.

Mamba akasema,  
"Nitakufunza."



Mamba akasema,  
"Sisi sasa ni  
marafiki. Usiogope."




Mamba akasema,  
"Mjomba ni  
mgonjwa. Anahitaji  
nyama ili apone."



Sokwe akaogopa sana.


Je, Mamba atamula?



Sokwe akataka  
kumtoroka Mamba.




Sokwe akapata  
wazo zuri.



"Nitautoa moyo  
wangu umpatie,"  
Sokwe akaahidi.




"Lakini moyo  
wangu uko mtini,"  
Sokwe akasema.



"Utauleta moyo  
wako?"  
Mambaakauliza.

Sokwe akamjibu,  
"Ndiyo."




Mamba akaogelea  
kutoka majini.

Sokwe akakimbilia  
kwenye miti.



"Wewe si rafiki  
yangu.  
Ulinidanganya!"  
Mamba akasema.



"Hatuko marafiki.  
Unataka kunila!"  
Sokwe akamjibu.